Kioo cha Lugha, Juz. 24(1), 84-100
Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v24i1.6

Dhima za Motifu "Paa" katika Riwaya ya *Nagona* (1990) na Diwani ya *Dhifa* (2022)

Nyamtondo Millium Mang'erere[1] *Neema George Mturo*[2]

Ikisiri

Makala hii imechunguza dhima za motifu "paa" katika riwaya ya *Nagona* (Kezilahabi, 1990) na diwani ya *Dhifa* (Kezilahabi, 2022). Lengo kuu la makala hii ni kufafanua dhima mbalimbali za motifu "paa" katika kazi tajwa na jinsi zinavyoibua motifu katika kuendeleza falsafa ya maisha. Data za makala hii zimekusanywa kwa njia ya uchanganuzi matini kutoka maktabani. Mjadala wa matokeo ya makala uliongozwa na Nadharia ya Mchomozo. Matokeo ya makala hii yameonesha kwamba mwandishi Kezilahabi ametumia motifu "paa" kama mtindo wa kuwasilisha mawazo ya kuendeleza falsafa ya maisha kwa kufanya ukiushi wa kisemantiki akitumia motifu "paa" katika riwaya ya *Nagona* kama motifu kuu inayosisitiza kuhusu suala la maisha kwa kuyalinganisha maisha ya binadamu na sifa za mnyama "paa". Hivyo, neno "paa" limetumika kama motifu pofu kwa kuchanganya dhana dhahania za neno "paa" katika diwani ya *Dhifa* kwa lengo la kuendeleza falsafa ya maisha.

1.0 Utangulizi

Makala hii imechunguza dhima za motifu "paa" katika riwaya ya *Nagona* na diwani ya *Dhifa.* Motifu imejikita katika kupambanua urudiaji wa vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi ili kuonesha miegamo ya waandishi katika kazi zao. Kwa kuzingatia urudiaji wa vipengele vya fani na maudhui vinavyotumiwa na mwandishi Kezilahabi, imeonekana kuwa na utofauti kwa sababu motifu "paa" imerudiwa kimchomozo kama Leech (1969) na Sympson (2004) wanavyosema kwamba, uchomozi unajipambanua kwa njia ya kuchopeka kwa makusudi kaida zilizozoeleka au kuweka mipangilio yenye ruwaza tofauti iliyo juu ya ile iliyozoeleka, kwa njia kama vile za uradidi au usambamba. Katika fasili ya uchomozi tunaona dhana hiyo ikihusishwa na kitendo cha kufanya ukiushi katika vipengele vyote vya kiisimu kwa kuhusisha darajia ya semantiki, sintaksia, mofolojia na fonolojia.

[1] Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Humanitia na Studi za Jamii, Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira. Tanzania. Barua pepe: nyamtorere@gmail.com

[2] Mhadhiri, Idara ya Humanitia na Studi za Jamii, Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira. Tanzania Barua pepe: neemamturo@yahoo.com

Suala la ukiukaji wa kaida za lugha zilizozoeleka ni la msingi katika kazi za fasihi kama inavyosisitizwa na Mulokozi (2017) kuwa lugha ndiyo kichocheo kikubwa kinachoweza kuleta athari kwa msomaji wa kazi ya fasihi. Anaongeza kwamba ukiukaji wa taratibu zilizozoeleka za lugha ndiyo huibua hisia za kumvutia msomaji na ukiukaji huo unaweza kuwa wa maana, sarufi na sauti.

Kwa kuzingatia dhana ya uchomozi jinsi inavyojipambanua katika vipengale vya kiisimu kama semantiki, fonolojia, sintaksia na mofolojia, tunaona ukiushi wa motifu "paa" katika riwaya ya *Nagona* na diwani ya *Dhifa.* Ukiushi huo unatokana na ukweli kwamba katika kamusi neno "paa" lina maana mbalimbali. Mosi, hurejelea *sehemu ya juu inayofunika nyumba*. Pili, humaanisha *mnyama wa porini anayefanana na mbuzi aliye mwembamba na mdogo*. Tatu, ni *kitendo cha kuchukua baadhi ya makaa ya moto kutoka kwenye jiko*. Nne, hurejelea *kitendo cha kuondoa magamba ya samaki kwa kuparuza kwa kitu*, na tano, ni *kitendo cha kuruka kuelekea angani*. Matumizi ya neno "paa" katika riwaya ya *Nagona* na diwani ya *Dhifa* yamesababisha mjengeko wa motifu kutokana na urudiaji wa vipengele vya fani au maudhui katika kazi za fasihi.

Dhima za motifu "paa" katika riwaya ya *Nagona* na diwani ya *Dhifa* ni muhimu kupambanuliwa ili kuondoa utata wa kiuchomozi unaojitokeza kama Miall na Kuiken (1994) wanavyoeleza kuwa kuna uhusiano baina ya mbinu ya ustaajabisho na uibuaji wa hisia mara tu msomaji anapokutana na matini yenye muundo kengeushi kwa kuwa sehemu maalumu katika ubongo inayohusika na uibuaji hisia hushughulishwa. Hivyo, katika riwaya ya *Nagona* na diwani ya *Dhifa* matumizi ya motifu "paa" huibua maswali kulingana na ukiushi wa kisemantiki unaojitokeza. Kwa kuzingatia ukiushi wa kisemantiki uliojitokeza katika motifu "paa", makala hii imefafanua bayana uchomozi wa dhima za motifu "paa" na jinsi zilivyoibua motifu katika riwaya ya *Nagona* na diwani ya *Dhifa.*

2.0 Dhana ya Motifu

Wamitila (2003) anaeleza kuwa motifu ni dhana, jambo au kipengele kinachojirudiarudia katika kazi ya fasihi. Kipengele hicho kinaweza kuwa cha kifani au cha kimaudhui. Hivyo, motifu ni dhana inayohusisha urudiaji wa vipengele vya fani au maudhui katika kazi za fasihi kwa makusudi fulani ya mtunzi.

Naye Ponera (2014) anafafanua kuwa motifu ni misuko au miegamo ambayo watunzi na watenzi wa kazi za fasihi huitumia kujenga miundo ya fani na maudhui ya kazi zao. Anasisitiza kuwa motifu hutumika kuonesha urudiaji wa wazo katika kazi ya fasihi. Aidha, kutokana na fasili hiyo tunaona wazi kwamba motifu imejikita katika kuonesha upekee wa mbinu za mtunzi katika kazi zake kwa kuzingatia uteuzi wa vipengele vya kifani au kimaudhui kwa kuvirudia kimatumizi ili kuibua maswali kwa msomaji.

Mulokozi (2017) na Ponera (2014) wanakubaliana kwamba motifu ni kipengele cha kifani au kimaudhui ambacho fanani na hata waandishi hukitumia

katika kuumba hadithi zao. Hivyo, kwa kurejelea maana hii tunaona wazi kuwa kipengele cha motifu kinaweza kutumika katika kazi za fasihi simulizi au andishi kwa kuwa kinachosisitizwa zaidi ni urudiaji wa vipengele vya fani na maudhui.

Kutokana na fasili hizo, tunaweza kusema kuwa motifu ni kipengele kinachohusisha urudiaji wa vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi kwa malengo maalumu kama vile kuendeleza dhamira, mtindo, msimamo, falsafa au ujumbe juu ya jambo fulani.

2.1 Aina za Motifu

Kwa mujibu wa Ponera (2014), kuna aina tatu za motifu. Aina ya kwanza ni motifu kuu. Aina hii ya motifu ndiyo inayotawala katika kazi za fasihi na ndicho kiini na mjengeko wa mawazo ya kazi husika. Motifu kuu hutumika katika kazi za fasihi kwa kuzingatia lengo kuu lililomsukuma mwandishi katika kuunda kazi yake. Motifu kuu hutumika kama nguzo katika kazi ya fasihi kwani inapoondolewa huweza kubadilisha mwelekeo wa kazi nzima na kuwa tofauti na ule aliokusudia mwandishi. Tofauti inaweza kutokea katika dhamira, uteuzi wa msamiati unaoibua ujumbe, uundaji wa wahusika wanaoibua dhamira au migogoro kulingana na malengo ya mtunzi.

Aina ya pili ni motifu kiambata. Hii ni motifu ambayo miegamo yake hutumiwa na waandishi ili kusaidia mjengeko wa motifu kuu na inahusisha miegemo mingine. Hivyo, motifu hii husaidia motifu kuu kuendelea kuwapo. Kutokana na nafasi yake, endapo motifu hii inaondolewa haiwezi kuleta madhara katika kazi husika, kwani hujikita zaidi katika kusaidia mjengeko wa motifu kuu.

Motifu pofu ni aina nyingine ya motifu. Hii inajengwa na mtunzi katika kazi yake kwa kukusudia au bila kukusudia, ili kusababisha mkanganyiko wa kifikra kwa hadhira. Mtunzi anaweza kutumia dhana za kidhahania, uigaji wa ghafla wa jambo katika usimulizi, na ujitokezaji wa tukio kwa namna inayochanganywa na matumizi ya fikra za kibwege. Ponera (2014) anasisitiza kwamba mara nyingi motifu pofu hutumika katika kazi zenye maudhui ya kifalsafa na matumizi hayo husababisha kutokuwa na maana ya wazi. Hivyo, ni dhahiri kuwa motifu pofu inahusisha mchomozo wa vipengele vya kiisimu kwa kufanya ukiushi katika vipengele vya fani na maudhui ili kuibua taharuki kwa msomaji.

3.0 Methodolojia za Utafiti

Makala hii imechunguza dhima za motifu ‘paa’ katika riwaya ya *Nagona* na diwani ya *Dhifa.* Watafiti wametumia mkabala mseto katika kukusanya na kuchambua data kulingana na malengo ya utafiti. Aidha, mkabala wa kitakwimu umetumika katika kutoa idadi ya ujitokezaji wa motifu “paa” katika kazi teule. Watafiti wametumia usanifu wa kifani katika kuteua kazi mbili zilizotumika katika makala hii ambazo ni riwaya ya *Nagona* na diwani ya *Dhifa* kwa lengo la kufafanua utofauti wa dhima za motifu ‘paa’. Mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumiwa kuteua kazi za Kezilahabi, riwaya ya *Nagona* na diwani ya *Dhifa* kwa

kuwa zina sifa ya urudiaji wa neno "paa" lililosababisha mjengeko wa motifu "paa".

Data za utafiti huu zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi matini kwa kusoma riwaya ya *Nagona* na diwani ya *Dhifa* na kuchambua motufu "paa". Mbinu ya kusimbisha maudhui ilitumika katika kupata data za utafiti huu. Katika hatua hii, kwanza, watafiti walisoma data zilizopatikana kutoka katika riwaya ya *Nagona* na diwani ya *Dhifa.* Pili, walitengeneza jedwali huku wakinukuu na kuchambua data. Mwisho, walitengeneza msimbo wa kutofautisha data kwa kuzingatia malengo ya utafiti ili kuunda ruwaza ya kimaudhui na kuzihusisha, kisha kuunda tafsiri mpya kimaudhui.

4.0 Kiunzi cha Nadharia

Makala hii ilitumia Nadharia ya Mchomozo ambayo iliasisiwa baada ya taaluma ya elimu mitindo kushika hatamu katika karne ya 20. Umaarufu wa nadharia hii ulitokana na matumizi ya vipengele viwili ambavyo ni ukiushi na usambamba kwani ndiyo viungo muhimu vitumikavyo katika kuunda matini za kifasihi. Nadharia ya Mchomozo iliasisiwa na Jan Mukarovsky akiwa mwanafunzi katika shule ya Prague, mwanzoni mwa karne ya 20. Nadharia hii iliungwa mkono na wanazuoni kama vile Roman Jakobson, Rene Wallek na Felix Vodicka.

Misingi ya Nadhariaya Mchomozo

Miall na Kuiken (1994) wanasema kwamba uchomozi huibua ustaajabisho, na ustaajabisho huo huwafanya wasomaji na wasikilizaji kupata taharuki kwa sababu hukutana na miundo iliyokengeuka ambayo inasababisha msomaji kukutana na maana ya ziada inayomsaidia kupata ujumbe uliokusudiwa na mtunzi. Makala hii inachunguza neno "paa" katika riwaya ya *Nagona* na diwani ya *Dhifa* linavyoleta ustaajabisho kulingana na matumizi yake, jambo ambalo linaweza kusababisha mkanganyiko kulingana na kuwapo kwa uelewa tofauti miongoni mwa wasomaji.

Pia, uchomozi huweza kuvuta hisia kutokana na ustaajabisho wa kile kilichochomozwa. Miall na Kuiken (1994) wanaeleza kuwa kuna uhusiano baina ya mbinu ya ustaajabisho na uibuaji wa hisia pale msomaji anapokutana na matini yenye muundo kengeushi. Hii inatokana na sehemu maalumu katika ubongo inayohusika na uibuaji hisia kushughulishwa. Hivyo, makala imechunguza riwaya ya *Nagona* na diwani ya *Dhifa* ili kujua namna msomaji anavyopata taharuki kulingana na matumizi ya neno "paa" kutokana na jinsi lilivyorudiwa kimatumizi na kuchomozwa kwa namna tofauti, hali inayoweza kumfanya msomaji kupata hisia za tafsiri za maana tofauti katika ubongo wake kutokana na uchomozi unaojitokeza.

Baada ya kuvuta hisia kwa kile kilichooneshwa, msomaji huweza kupata muda wa kutafakari kile kilichokengeushwa, ili abaini maana iliyokusudiwa na mwandishi kwa kushughulisha ubongo wake. Miall na Kuiken (1994) wanadokeza kuwa kwa vile uchomozi hujitokeza katika vipengele vinavyoshabihiana vya

kisauti, kisarufi na kimaana, husababisha kuwapo kwa kipindi cha kujikumbusha, hivyo, hutumia muda. Kwa hiyo, baada ya msomaji kuvuta hisia na tafsiri za maana tofauti katika ubongo wake kutokana na uchomozi wa motifu "paa" katika kazi mbili za mwandishi Kezilahabi, huanza kutafakari ili kubaini dhamira ya mwandishi Kezilahabi ilikuwa ni ipi katika kutumia neno "paa" kutoka katika matumizi ya kawaida yaliyozoeleka.

Kutokana na utafiti wa Peer (1986) athari za uchomozi huwagusa watu wa aina zote wakiwamo wasomi na wasio wasomi, hivyo, uchomozi una kawaida ya kuathiri kundi kubwa la watu. Kwa kuzingatia hoja ya Peer, "paa" katika riwaya ya *Nagona* na diwani ya *Dhifa* huweza kuleta athari katika uga wa fasihi na jamii kwa ujumla, kutokana na neno hili kuzua taharuki zinazosababisha wasomaji kushindwa kubaini lengo la mwandishi au usahihi wa matumizi ya neno hili kulingana na uchomozi.

5.0 Dhima za Motifu "Paa" katika Riwaya ya *Nagona* na Diwani ya *Dhifa*

Katika sehemu hii tumewasilisha data zinazohusu dhima za motifu "paa" katika riwaya ya *Nagona* na diwani ya *Dhifa* na kufanya uchambuzi ili kukamilisha lengo la makala. Katika uwasilishaji, alama (✓) inawakilisha dhima zilizojitokeza na alama (×) inawakilisha dhima ambazo hazijajitokeza katika kazi husika.

Jedwali Na. 1: Dhima za Motifu "Paa" katika Diwani ya *Dhifa*

Dhima Zisizo na Ukiushi wa Kisemantiki	**Alama**	**Dhima zenye Ukiushi wa Kisemantiki**	**Alama**
"Paa" imetumika kama sehemu ya juu inayofunika nyumba	✓	"Paa" imetumika kama lugha ya picha inayoashiria maisha	✓
"Paa" imetumika kama mnyama wa porini anayefanana na mbuzi	×	"Paa" imetumika kama anometopeya	✓
"Paa" imetumika kama kitendo cha kuchukua baadhi ya makaa ya moto kutoka kwenye jiko	×	"Paa" imetumika kama mtindo	✓
"Paa" imetumika kama kitendo cha kuondoa magamba ya samaki kwa kuparuza kwa kitu	×	"Paa" imetumika kama taswira ya kitu kinachotokea kwa ghafla na kupotea bila kutarajia	✓
"Paa" imetumika kama kitendo cha kuruka kuelekea angani	×		×

Jedwali Na. 2: Dhima za Motifu "Paa" katika Riwaya ya *Nagona*

Dhima Zisizo na Ukiushi wa Kisemantiki	**Alama**	**Dhima zenye Ukiushi wa Kisemantiki**	**Alama**
"Paa" imetumika kama sehemu ya juu inayofunika nyumba	✓	"Paa" imetumika kama lugha ya picha inayoashiria maisha	✓
"Paa" imetumika kama mnyama wa porini anayefanana na mbuzi	✓	"Paa" imetumika kama mlio unaoashiria ishara ya kifo	✓
"Paa" imetumika kama kitendo cha kuchukua baadhi ya makaa ya moto kutoka kwenye jiko	×	"Paa" imetumika ikirejelea mhusika jasiri	✓
"Paa" imetumika kama kitendo cha kuondoa magamba ya samaki kwa kuparuza kwa kitu	×	"Paa" imetumika kama nidaa	✓
"Paa" imetumika kama kitendo cha kuruka kuelekea angani	×	"Paa" imetumika ikirejelea dhana ya ujaala	✓
		"paa" imetumika ikirejelea dhana ya ukweli "paa" imetumika kurejelea	✓
		kurejelea msichana	✓

5.1 Ufafanuzi wa Dhima za Motifu "Paa" katika Riwaya ya *Nagona* na Diwani ya *Dhifa*

Sehemu hii imefafanua dhima za motifu "paa" zilizojitokeza katika riwaya ya *Nagona* na Diwani ya *Dhifa.*

5.1.1 Motifu "Paa" kama Sehemu ya Juu Inayofunika Nyumba

Katika diwani ya *Dhifa* data zimeonesha kuwa mwandishi Kezilahabi ametumia motifu "paa" akirejelea sehemu ya juu inayofunika nyumba, ambapo data zimeonesha sehemu mbalimbali kama vyooni, kuta za ikulu, khanga na tisheti. Nukuu kutoka katika diwani ya *Dhifa* (uk. 6), shairi la "Mafuriko" inasema:

> Juu ya kuta vyooni, maofisini, madarasani,
> Juu ya "**paa**" za nyumba, Kuta za ikulu,
> Na juu ya khanga na tisheti.
> Nitaandika wimbo huu,
> Juu ya vidonda vya wakulima,
> Na usaha wa jasho lao….

Kwa kuzingatia nukuu iliyotolewa kutoka katika diwani ya *Dhifa* hapo juu, mwandishi ametumia motifu "paa" akirejelea sehemu ya juu inayofunika nyumba

ili kuonesha sehemu mbalimbali ambazo ataandika wimbo wa malalamiko. Mwandishi ameonesha hisia zake kuhusiana na suala zima la ugumu wa maisha kwa tabaka la chini hasa wakulima. Aidha, anaonesha sehemu mbalimbali atakazoandika wimbo unaoashiria kilio juu ya ukandamizaji wa tabaka la chini. Mwandishi anaonesha sehemu kama vyooni, ofisini, madarasani, juu ya paa na kuta za ikulu, kwa kawaida ni ngumu kuandika katika mazingira hayo. Hivyo, kulingana na Nadharia ya Mchomozo kuhusiana na matumizi ya ukiushi wa maneno, mwandishi ametumia motifu "paa" kama sehemu ya kuandika malalamiko yake ilhali neno "paa" hutumika kama sehemu ya juu inayofunika nyumba.

Pia, mwandishi ametumia motifu "paa" kurejelea sehemu ya juu inayofunika nyumba katika riwaya ya *Nagona* kuunda matukio katika ufanikishaji wa dhamira kwa msomaji. Mfano ufuatao kutoka katika riwaya ya *Nagona* unafafanua:

> Nilistuka niliposikia milio ya bundi juu ya **paa** la nyumba niliyokuwa nikilala (uk. 41).
>
> Kama mtu aliyekuwa akinitazamia, alitabasamu halafu polepole akakilaza tena. Huku akitazama **paani** aliuliza... (uk. 42).
>
> "Mwache babu yako apumzike kidogo, usimsemeshe sana akiwa na njaa". Nilisikitika kutoka nje "katika uhai wake wewe ndiye daima ulikuwa karibu naye, Bado hujatosheka tu na maneno yake. Mwache akae nami", babu alisema, "Bila yeye nisingekuwa katika hali niliyonayo ...", kisha akasema maisha hayatakwisha bali watu waishio (uk. 43).

Kwa kurejelea nukuu hizo kutoka katika riwaya ya *Nagona*, mwandishi ametumia motifu "paa" akirejelea sehemu ya juu inayofunika nyumba. Katika kulidhihirisha hilo anaonekana mhusika aliyekuwa katika ndoto lakini akashtushwa na mlio wa bundi juu ya paa la nyumba aliyokuwa akilala. Nadharia ya Mchomozo inasisitiza kuhusu kuvuta hisia na kuibua ustaajabisho pale msomaji anapokutana na motifu "paa" katika matumizi yasiyo ya kawaida; hupata muda wa kutafakari kulingana na kile kinachochomozwa. Katika nukuu iliyotolewa, mwandishi ametumia neno "paa" ili kuonesha jinsi mhusika alivyokuwa akiota na kushtushwa na kiumbe chenye jina la paa. Hapa mwandishi alitumia motifu "paa" kuonesha dhamira ya umuhimu wa wazee na suala la kifo kutokana na maongezi yaliyokuwa yanaendelea kati ya mhusika na Babu yake chumbani mpaka mauti yalipomkuta.

5.1.2 Motifu "Paa" kama Lugha ya Picha Inayoashiria Dhana ya Maisha

Katika kazi teule, mwandishi ametumia motifu "paa" kuelezea dhana ya ukweli kuhusu maana ya maisha. Katika diwani ya *Dhifa* mwandishi ametumia dhana ya motifu "paa" kama kivuli kinachoashiria dhana nzima kuhusu maisha. Nukuu kutoka katika shairi la "Wakati Fulani" (uk. 21) inaeleza:

Wakati fulani twasubiri kuche,
Kama mtoto mdogo aliyesikia,
Embe bivu zito likidondoka usiku,
Wakati fulani twamsaka **Paa** gizani"
Kujua na kutojua wakati,
Kutegemea na kutotegemea
Twaishi kwa kujikongoja
Tukisema kimoyomoyo
Kwa akili sinzinzi
Wakati fulani utafika,
Hadi wakati wa kifo.
Kutojua ni kujua.
Kuishi ni kufa.

Nukuu hapo juu inaonesha kwamba mwandishi ametumia motifu "paa" kama lugha ya picha kufafanua kuwa kuna wakati binadamu wanamsaka "paa" gizani ambapo motifu "paa" inarejelea picha nzima ya maisha. Kwa kuzingatia Nadharia ya Mchomozo inayosisitiza ukiukaji wa matumizi ya kawaida katika maneno, imedhihirika kuwa mwandishi amefanya ukiushi wa kisemantiki kwa neno "paa" na kulitumia katika miktadha tofauti kama lugha ya picha inayorejelea maisha. Matumizi ya lugha ya picha katika kazi za fasihi, kwa mujibu wa Njongu na Chemirah (1999), hutumika ili kujenga picha fulani katika akili ya msomaji au msikilizaji. Picha inayotumika hutegemea ina ushawishi kiasi gani kulingana na nguvu ya taswira ya neno lililotumika. Nukuu iliyotolewa inaonesha jinsi binadamu anavyopambana kuyasaka maisha lakini anakutana na misukosuko mbalimbali mpaka anafikia hatua ya kukata tamaa na kuona maisha hayana maana kwani binadamu anaishi kwa kutojua kuishi ni kufa.

> Pia, katika riwaya ya *Nagona* mwandishi ametumia motifu "paa" kurejelea dhana ya maisha. Dhana ya maisha imechukua nafasi kubwa katika riwaya ya *Nagona.* Katika kusawiri uhalisia wa namna mwandishi anavyoyachukulia maisha, ametumia motifu "paa" kama lugha ya picha inayoashiria maisha. Mwandishi anasema:
>
> "Hawa wote walimsaka **paa,** lakini mwisho wao umekuwa huu, msichana alitwambia". Nabii aliachama, Mfalme alishika tama, Mfuasi alishika kidevu, na Mtenzi kilemba kilimlegea, sasa nambieni! "Bado mnataka kumsaka Paa?" Kimya kilifuata.
>
> Uwaonao katika duara hili ni kikundi kidogo tu cha waliokuwa wabishi katika usakaji wa njia. Yule pale ni Plato, na yule ni Socrates. Huyu hapa ni Aristotle ... ilibidi wafungwe vitambaa machoni kwa sababu walikuwa karibu kukata tamaa" (*Nagona,* 30 - 31).

Katika nukuu iliyotolewa hapo juu, mwandishi ametumia neno "paa" akirejelea dhana ya maisha; ameonesha watu mashuhuri ambao ni wanafalsafa, Socrates, Plato na Aristotle. Mwandishi ameonesha wazi kuwa maisha hayana maana hata

kwa watu maarufu na viongozi waliopambana na kuacha historia katika jamii lakini mwisho wake wameishia kwenye mvunjiko ambao ni kifo.

Hoja hii inaungwa mkono na Mungah (1999) katika utafiti wake aliofanya kuhusiana na riwaya za *Nagona* na *Mzingile* na kuonesha msimamo wa mwandishi jinsi anavyoyatazama maisha kuwa hayana maana. Matokeo hayo yanajidhihirisha wazi yakihusianishwa na Nadharia ya Mchomozo inayasisitiza ukiushi wa kisemantiki. Kwa hiyo, motifu "paa" imetumika katika riwaya ya *Nagona* ili kusawiri uhalisia wa maisha ya binadamu na hivyo kuibua matumizi mapya ya motifu "paa" katika lugha kwa kutumia neno "paa" kumaanisha maisha hayana maana.

5.1.3 Motifu "Paa" kama Onomatopoeia

Data zimeonesha kuwa mwandishi ametumia neno "paa" kama anometopeya. Kwa kawaida anometopeya hutumika kuiga sauti ya kitu fulani. Hivyo, mwandishi ametumia motifu "paa" akirejelea mlio unaoashiria hatari inayosababisha kifo, ikiwa ni ishara ya roho inapotoka katika mwili wa binadamu. Hii inadhihirika katika shairi la "Maisha" (uk. 40), mwandishi anaeleza:

> Ulimwengu, kizaazaa, umekeaa, kibaabaa,
> Na maisha, ya **paa paa,** yamejaa, hadaadaa,
> Binadamu, twataataa, kwa fadhaa, twakaakaa
> Maisha, nyondenyonde, Kila saa, twaduwaaduwaa
> Miguu, nyakanyaka, ' meshupaashupaa
> Na sura, nyong'onyong'o. 'mechakaa, mesinyaa...
> Miili, nyanga'nyang'a, twazubaa, twashaashangaa
> Hae! Dunia tambara bovu asimamaye huanguka

Kwa kuzingatia mifano iliyotolewa, matokeo yameonesha kuwa mwandishi ametumia motifu "paa" kama kiashirio cha kuonesha jinsi maisha yalivyojaa matatizo mbalimbali ambayo husababisha kifo. Hii inadhihirisha kuwa maisha ya binadamu hayaeleweki na kifo hutokea ghafla bila kutarajia. Nadharia ya Mchomozo inasisitiza ukiushi wa kisemantiki katika kuelezea fikra. Kwa hiyo, matokeo yameonesha kwamba mwandishi ametumia "paa" kama mlio unaoashiria mwenendo halisi wa maisha ya mwanadamu hadi kusababisha kifo. Wamitila (2008) anasisitiza kuwa onomatopoeia hutumika pale ambapo neno fulani hutumika kuiga sauti ya kitu fulani. Kwa upande wa Kezilahabi ametumia motifu "paa" kama mlio unaoashiria uhalisia wa maisha ya hofu yanayosababisha kifo, kwa kusawiri maisha kuwa hayana maana na kuyalinganisha na tambara bovu.

Kwa kuzingatia mifano hiyo, tunaona mwandishi ametumia motifu "paa" kwa kukiuka kaida zilizozoeleka za lugha. Neno "paa" limetumika kama kiashirio cha kuonesha jinsi maisha yalivyojaa matatizo mbalimbali ambayo husababisha kifo. Anaendelea kusisitiza kwamba maisha yanahitaji uvumilivu kwani ukiwa mzembe ni rahisi kukata tamaa. Hivyo, kwa kuzingatia Nadharia ya Mchomozo, ni

dhahiri mwandishi amefanya ukiushi wa kisemantiki wa kutumia motifu "paa" katika miktadha tofauti na iliyozoeleka.

Halikadhalika, katika riwaya ya *Nagona,* data zimeonesha mwandishi ametumia motifu "paa" akirejelea mlio unaoashiria dhana ya kifo. Mwandishi ametumia motifu "paa" kama mlio wenye ishara ya kifo ili kuelezea kwa kina dhamira aliyonayo kwa hadhira kwa kutumia lugha ya picha kama nukuu ifuatayo inavyoonesha:

> "Hamjaona lolote. Huu ni mwanzo tu," alitwambia. Mara tulisikia mlio "Oo! Paa!" tulimsikia mtu akilialia Karibu naye tuliona pandikizi la mtu lilikuwa uchi liliinua shoka juu na kukata shingo lake". Hatukusikia tena milio (uk. 30).

> "Huyo pia alimsaka paa. Leo asubuhi alishindwa kumshika ", Yule msichana alitwambia "alikuwa mwanafalsafa mashuhuri"(uk. 25).

Kwa kuzingatia nukuu hapo juu kutoka katika riwaya ya *Nagona,* mwandishi ametumia motifu "paa" akiashiria mlio wa maisha uliobeba dhana ya kifo, ambapo mwandishi ameonesha wazi mlio uliosikika na baadaye shoka lilikata shingo na ule mlio haukusikika tena. Hivyo, matokeo yameonesha kwamba ilikuwa ishara ya mlio ambao ni sababu ya kifo kwa binadamu kwani suala la kifo ni la kila mtu. Hata kama atafanikiwa kufanya mambo mengi katika kuyasaka maisha lakini mwisho wake ni kifo. Gaudioso (2014) anafafanua dhana ya "pa!" kwa kuelezea kuwa hurejelea mlio wa maisha kwa kutumia lugha pasipo kutumia maneno. Halikadhalika, mbali na dhana ya "paa" na "pa" kutofautiana katika maana na wakaa lakini katika msikiko wa mlio hurejelea maana sawa. Hivyo, matokeo yameonesha kuwa motifu "paa" imetumika kama mlio unaoashiria maisha ya kifo. Hoja hii inashadidiwa na Nadharia ya Mchomozo kwa sababu mwandishi ametumia motifu "paa" kwa kukiuka kaida iliyozoeleka kimaana na kutumia katika matumizi tofauti akirejelea mlio unaoashiria dhana ya kifo inayosababisha taharuki kwa msomaji. Ukiukaji huo wa kisemantiki unadhihirika zaidi pale mhusika msichana anapowaonesha wahusika njia iliyojaa mifupa ya wafu na baadaye wakasikia mlio "paa". Ni dhahiri kuwa mlio huo ulikuwa unarejelea kifo kwa kutumia motifu "paa".

5.1.4 Motifu "Paa" kama Mtindo wa Kuonesha Upangilifu wa Vina katika Shairi

Katika diwani ya *Dhifa* mwandishi ametumia motifu "paa" kuonesha upekee wake katika utunzi kwa kutumia neno "paa" katika upangilifu wa vina katika shairi. Mpangilio huo humvutia msomaji ili asichoke kusoma kazi yake kama inavyoonekana katika shairi la "Maisha" (uk. 40):

> Maisha nyondenyonde, kila saa, twaduwaduw**aa**
> Miguu, nyakakanyaka, tukikaa, 'meshup**aa**shu**paa**.

Kutokana na nukuu hapo juu, imebainika kwamba mwandishi ametumia neno “paa” katika ubunifu wa upangilifu wa vina katika shairi. Lengo la kufanya hivyo ni kumvutia msomaji kwa njia ya pekee kwa kutumia upangilifu wa takriri irabu “a”. Wamitila (2003) anasisitiza juu ya suala la mtindo kuwa huhusisha mbinu au sifa inayomwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe wake ambapo ubunifu huo unaonekana katika uteuzi wa msamiati, taswira, na mbinu nyingine kwa lengo la kuonesha ubora wa kazi husika. Nadharia ya Mchomozo inahusisha suala la mtindo kuchukuliwa kama kitendo cha kwenda nje na taratibu zilizozoeleka za lugha, hivyo, katika diwani ya *Dhifa "*paa” imetumika kama mtindo kwa kutumia motifu “paa” ili kukidhi upangilifu wa vina katika shairi na kuibua dhamira ya maisha kwa kutumia irabu “a”.

Vilevile, katika riwaya ya *Nagona* data zimeonesha mwandishi ametumia motifu “paa” kama mtindo wa kuelezea fikra zake kwa hadhira iliyokusudiwa, ambapo tunaona mwandishi ametumia motifu “paa” kimchomozo, yaani kwa wingi wa matumizi yanayoibua taharuki kwa msomaji. Mwandishi ametumia motifu “paa” mara 51 katika riwaya yake ya *Nagona*. Matokeo yameonesha mwandishi ametumia motifu “paa” kama mtindo wa kuelezea fikra zake kwa hadhira iliyokusudiwa, ambapo ametumia motifu “paa” kimchomozo, yaani kwa wingi wa matumizi yanayoibua taharuki kwa msomaji. Hivyo, mwandishi ametumia ubunifu wa kutumia mchomozo wa motifu “paa” kama mtindo wa kuelezea mawazo yake. Wamitila (2008) anabainisha kuwa, katika suala la mtindo kinachoangaliwa ni uteuzi wa msamiati, miundo, sentensi, matumizi ya tamathali za semi na jazanda, usawiri wa wahusika, motifu na dhamira. Hivyo, kwa kuzingatia Nadharia ya Mchomozo, matokeo yanaonesha kuwa mwandishi ametumia motifu “paa” kwa kukiuka kaida zilizozoeleka za lugha na kuunda matumizi mapya kama nadharia inavyosisitiza ikiwa ni lengo la kimtindo katika kuwasilisha dhana ya maisha.

5.1.5 Motifu “Paa” kama Taswira ya Kitu Kinachotokea na Kutoweka Ghafla

Mwandishi ametumia motifu “paa” katika diwani ya *Dhifa* kama taswira inayoingia akilini mwa msomaji kulingana na matumizi ya neno “paa” katika miktadha iliyotumika kwa kurejelea suala la uhai na kifo jinsi linavyotokea na kutoweka ghafla pasipo kutarajia. Katika shairi la “Maisha” (uk. 40), mwandishi anaeleza:

> Ulimwengu, kizaazaa, umekeaa, kibaabaa,
> Na maisha, ya **paa paa,** yamejaa, hadaadaa,
> Binadamu, twataataa, kwa fadhaa, twakaakaa

Katika nukuu hii, mwandishi ametumia motifu “paa” katika diwani ya *Dhifa* kama taswira ambayo inaingia akilini mwa msomaji kulingana na matumizi ya motifu “paa” katika miktadha iliyotumika kwa kurejelea kitu ambacho kinatokea na kutoweka ghafla bila kutarajia. Senkoro (2011) anasisitiza kuwa taswira ni

matumizi ya lugha yanayopambanuliwa na uteuzi wa maneno, ulinganifu na udhahiri wa maelezo wenye kuhusisha na kujumuisha dhana mbalimbali tofauti ndani ya dhana moja ili kuleta taswira na athari maalumu katika mawazo ya msomaji. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Mchomozo inayosisitiza matumizi ya kawaida ya maneno kutumika katika miktadha tofauti na iliyozoeleka, matokeo yanaonesha kwamba katika diwani ya *Dhifa* mwandishi ametumia neno "paa" kama taswira inayojengeka akilini mwa msomaji ikirejelea kitendo cha kitu kinachotokea na kutoweka katika mazingira ya ghafla. Hivyo, kwa kutumia Nadharia ya Mchomozo matokeo yanaonesha kwamba mwandishi amefanya ukiushi wa kisemantiki kwa kutumia motifu "paa" kama taswira inayoashiria mfano wa kitu kinachotokea ghafla na kutoweka kama yalivyo maisha ya binadamu. Kwa hiyo, kwa kurejelea dhima za neno "paa" katika kamusi, ni dhahiri kwamba mwandishi amefanya ukiushi wa kisemantiki kwa kutumia motifu "paa" kama kitu kinachotokea na kutoweka ghafla. Matumizi hayo ya motifu yanaibua maswali kwa msomaji kwani katika uhalisia wa maisha, binadamu anazaliwa pasipo kutarajia na kutoweka kwake duniani hakutabiriki.

5.1.6 Motifu "Paa" kama Mhusika Jasiri

Mwandishi ametumia motifu "paa" akimrejelea mtu jasiri ambaye anaaminika katika jamii, ana uwezo mkubwa na akili nyingi za kuwaongoza watu wengine kwenye jamii katika kuisaka dhana ya ukweli kuhusu maisha. Katika riwaya ya *Nagona* (kur. 33 - 35), mwandishi anaeleza:

> **Paa** alitoa mkono wake kuuelekeza baoni tulishangaa, lakini hakusema neno ... mchezo wa marudiano **paa** alishinda (uk. 33).
>
> "Hakikisha kibuyu chako kina maji," **paa** alimwambia. "Bado kiu ingaliko, na wasakaji wengi watapita njia hii". **Paa** aliendelea kuongoza njia hadi tulipofika machungani (uk. 35).

Katika mifano hapo juu, mwandishi ametumia motifu "paa" akirejelea shujaa na mtafuta njia wa kuelekeza kweli ya falsafa ya uhalisia wa maisha, ambapo tunaona paa aliongoza njia na kuwatia moyo wahusika ambao ni Mtume na Nabii katika kuusaka ukweli na kuwasisitiza kuwa kweli imo katika kimya. Vilevile, matokeo yanaonesha motifu "paa" imetumika kama mhusika asiyekubali kushindwa na anaaminika katika jamii yake, ndiyo sababu mfalme aliweka shindano la kucheza bao ili apime uwezo wa mhusika Mtenzi na Nabii kama wana uwezo wa kumshinda paa aliyekuwa akiaminiwa na mfalme. Kwa kuzingatia Nadharia ya Mchomozo inayosisitiza kuhusu ukiushi wa kisemantiki katika kazi za fasihi ndivyo ilivyojitokeza katika riwaya ya *Nagona* ambapo mwandishi ametumia motifu "paa" akimrejelea mhusika jasiri.

5.1.7 Motifu "Paa" kama Dhana ya Ukweli

Mwandishi Kezilahabi ametumia motifu "paa" akirejelea ukweli halisi wa maisha

kwa kutumia ubunifu wa ishara unaojikita katika kuonesha ni kwa jinsi gani kuna changamoto mbalimbali alizozipitia mhusika “paa” katika kusaka ukweli kuhusu dhana ya maisha. Katika riwaya ya *Nagona* anaeleza:

> Tunamtafuta **paa**. Umemwona akipita. Sasa hapana shaka moyoni mwangu kuwa wewe ndiye **paa** mmtafutaye alipita hapa. Mkivuka tu upande mwingine mtaona nyayo zake na hazitapotea tena kwa sababu ng'ambo hiyo uwongo umejitenga (uk. 28).
>
> “Aliinua mikono yangu juu akasema “shujaa msaka **paa”** (uk. 29).
>
> Tumesikia ushujaa wenu na tunahofu kuwa huenda mkafanikiwa kumshika **paa** ambaye amewashinda wengi (uk. 30).

Kwa kuzingatia nukuu zilizotolewa, matokeo yameonesha jinsi mwandishi alivyokuwa mbunifu katika matumizi ya motifu “paa” ambapo ametumia motifu “paa” akirejelea ukweli ambao umo ndani ya maisha na ukweli huo uliwashinda wengi. Hoja hii inaunga mkono hoja ya Mbatiah (2018) aliyeeleza kuwa neno “paa” hurejelea dhana ya ukweli baada ya kufafanua sitiari tatu ikiwamo “paa”, Mwanga na Nagona. Kwa hiyo, matokeo yanaonesha wahusika waliokuwa wakimtafuta “paa” na kuthibitishiwa kwamba wakiona nyayo zake hawatapotea tena kwani uongo umejitenga. Hivyo, matokeo yanathibisha wazi kuwa motifu “paa” imetumika kurejelea ukweli. Pia, kwa kurejelea msisitizo wa Nadharia ya Mchomozo ni dhahiri motifu “paa” imetumika katika miktadha tofauti ambapo neno “paa” limetumika kama ukweli na kufanya msamiati huu kuibua maana nyingine ya zaida kama Ponera (2014) anavyosisitiza kuwa katika kazi za sanaa kuna maana fiche na wazi na maana fiche ndiyo huchukua nafasi kubwa, hivyo, uibuaji wa maana fiche huhitaji uhusishaji wa miktadha maalumu ili kuelewa maana ya neno.

5.1.8 Motifu “Paa” kama Mnyama

Mwandishi Kezilahabi ametumia motifu “paa” akirejelea mnyama ambaye ni jamii ya mbuzi anayeishi porini. Mpangilio wa uundaji wa matukio na mshikamano wa matukio unadhihirisha kile alichokikusudia mwandishi kimfikie msomaji. Hilo linajidhihirisha katika riwaya ya *Nagona* kama ifuatavyo:

> Nilipoangalia kwa uangalifu pale tulipokuwa, niliona nyayo zilizoelekea kuwa za mnyama. Nilimtazama yule mwanamke. Alitabasamu kisha akasema, “Ni **“paa”**… ametoka wapi? Katika msitu uliokuwa wewe yaelekea ulimkurupusha”. Alielekeza macho yake kwenye jiwe, niliona upinde na mishale miwili.
>
> Mwanamke alinitazama. **“**Mwindaji fulani alipita hapa**”**? …. Uliwinda kipepeo wa kila aina ya rangi. Siku moja ulimfuata kipepeo mwenye rangi nyingi hadi katikati ya msitu katika kichaka kimoja alikurupuka **paa** aliyekustua” (uk. 11).

Kwa mujibu wa nukuu hizo, mwandishi Kezilahabi ametumia motifu "paa" akirejelea mnyama katika mazingira ambayo mnyama "paa" anapatikana, kwa mfano; mazingira ya msituni; pia, mwandishi ameonesha nyayo alizopita mnyama "paa". Vilevile, mwandishi ametumia mhusika mwindaji ambaye kazi yake ni kuwinda wanyama. Hivyo, kutokana na maelezo hayo motifu "paa" imetumika kama mhusika mnyama ambapo tunaona alimkurupusha mhusika katika msitu aliokuwa. Pia, mhusika aliyekuwa msituni akifuatilia vipepepeo alimuona mnyama aina ya "paa" aliyekurupuka kutoka kichakani, hivyo, mwandishi amemchora "paa" kama mnyama ambaye anaishi msituni.

Kama ilivyoelezwa, Nadharia ya Mchomozo inasisitiza ukiushi wa kisemantiki unaohusisha ugeuzaji wa maana ya msingi, na kuwa maana ya ziada hutegemea muktadha. Kwa kuzingatia ugeuzaji wa maana iliyozoeleka kuonekana katika miktadha tofauti, mwandishi ametumia motifu "paa" kama mnyama lakini akirejelea maana nyingine ambayo ni ukweli kuhusu maisha.

5.1.9 Motifu "Paa" kama Msichana

Mwandishi ametumia neno "paa" akirejelea msichana ambaye ni mrembo na mwenye sifa zote za kuwa mke atakayemsaidia msakaji anayetafuta ukweli kufanikisha lengo lake. Hii ni kutokana na wazazi wake kuwa na imani kuwa kupata mke ni ishara itakayoonesha ukomavu wa akili wa kijana wao na kudhihirisha ana uwezo wa kupambana, kwa kuwa ameshakuwa mtu mzima anayejitambua, hivyo, anaweza kusaka ukweli na kuufahamu. Mwandishi anaeleza katika riwaya ya *Nagona*:

> Mfunue **paa** wako". Nilisogea mbele polepole. Nilimfunua **paa** kuanzia kichwani hadi miguuni. Alikuwa msichana mzuri ambaye hajapata kuonekana. Nilipomfunua tu mziki ulilia (uk. 34).
>
> Msichana alikimbia akamkumbatia. Machozi yalimlengalenga yule mwanamke, aliponikaribia akasema "Huyu ndiye **paa** niliye kwambia umsake. Umeanza kuwa mtu mzima na karibu utajua wajibu wako katika dunia hii" (uk. 36).

Kutokana na mifano hiyo, mwandishi ametumia motifu "paa" akirejelea msichana ambaye yuko tayari kuwa mke atakayeonesha ukomavu wa shujaa anayesaka ukweli kuwa ameshakuwa mtu mzima na ana uwezo wa kupambana kuusaka ukweli kuhusu maisha. Kwa kuyadhihirisha hayo, nukuu imeonesha shujaa akimfunua "paa" ambaye ni msichana mrembo. Kulingana na maelezo hayo, ni wazi neno "paa" limebadilika kimatumizi. Kama Nadharia ya Mchomozo inavyosisitiza kuhusu ukiushi wa kisemantiki, mwandishi ametumia motifu "paa" kurejelea msichana ambapo si kawaida ya neno hili kutumika katika muktadha huo.

5.1.10 Matumizi ya Motifu “Paa” Kurejelea Kutokuwapo kwa Dhana ya Ujaala

Kwa kutumia motifu “paa” mwandishi ameonesha kuwa suala la ujaala katika maisha ya binadamu halipo kutokana na kutokuwa na imani juu ya uwepo wa Mungu. Hii inatokana na maisha ya binadamu kukumbwa na matatizo mbalimbali yanayosabibisha kifo. Hivyo, mwandishi Kezilahabi ametumia motifu “paa” katika kurejelea ukweli kuhusu maisha na kutokuwa na imani kunadhihirika kwani anaamini hata binadamu kuwapo duniani ilitokea kama ajali kama anavyoeleza katika ya *Nagona*:

> Walitazamana, halafu Mtume alimtazama Nabii akasema, nilikwambia ndiye yeye! Ndiye … ndiye ... wote wawili walipiga kelelele, tumefurahi sana kukuona, Nabii alisema ..... kwa sasa tumekutambua tuko tayari kufuatana nawe. “Huyu **Paa** mmtafutae alipita hapa”
>
> “Hawa wote walimsaka **paa** mwisho wao umekuwa huu”, msichana aliniambia. Nabii aliachama, Mtume alishika kidevu na Mtenzi kilemba kilimlegea. (uk. 27).

Kwa kuzingatia nukuu hizo ni wazi kuwa baadhi ya viongozi wa dini hawana imani na Mungu kwani na wenyewe walikuwa katika safari ya kuusaka ukweli wa maisha. Nukuu inaonesha mhusika Mtume na Nabii walikuwa katika safari ya kuusaka ukweli na walipooneshwa ukweli wa maisha ya kifo wakaondoa imani ya uwepo wa Mungu wakihoji kama Mungu yupo kwa nini wanadamu hupitia matatizo katika maisha.

Ponera (2014) anasisitiza kuwa ujaala ni hali ya kunasibisha kuwapo kwa viumbe waliomo duniani na uwezo wa Mungu. Hivyo, kwa kuongozwa na Nadharia ya Mchomozo ni dhahiri neno “paa” limetumika kurejelea kutokuwepo kwa dhana ya ujaala katika maisha ya binadamu. Mwandishi alipokuwa akimuongelea malaika Gabriel na kurejelea Vita vya Pili ambapo ukweli wa kifo ulitokea, Mtume alishangaa na Nabii akakiri kuufuta ukweli huo. Ni dhahiri imani ya Mungu imeonekana kutoweka kutokana na matatizo yanayomkumba mwanadamu na suala la kifo. Kwa kuzingatia maelezo hayo motifu “paa” imetumika katika miktadha ambayo haijazoeleka kupitia safari ya kumsaka “paa”. Hivyo, nafasi ya Mungu ikaonekana haina msaada baada ya kugundua ukweli. Ndiyo maana Nabii alishangaa na Mtume alishika kidevu baada ya kujua ukweli.

5.1.11 Motifu “Paa” kama Nidaa

Katika makala hii, data zimeonesha motifu “paa” imetumika kama nidaa kulingana na jinsi mwandishi Kezilahabi alivyoitumia katika riwaya ya *Nagona.* Mwandishi ametumia alama ya mshangao katika neno “paa” kwa kuonesha mshangao wa mlio uliosikika. “Hamjaona lolote. Huu ni mwanzo tu”, alitwambia. Mara tulisikia mlio “Oo! **Paa**! 2”

Katika nukuu, ni wazi kuwa motifu “paa” imetumika kama nidaa kulingana

na jinsi mwandishi alivyotumia katika riwaya ya *Nagona.* Matumizi hayo siyo ya kawaida katika lugha kama Nadharia ya Mchomozo inavyosisitiza suala la ukiushi kuwa ndiyo nguzo kuu ya mchomozo. Hivyo, mwandishi ametumia alama ya mshangao katika motifu "paa" kwa kuonesha mshangao wa mlio uliosikika. Senkoro (2011) anabainisha kuwa nidaa ni msemo ambao unaonesha kushangaa au kushangazwa na jambo fulani, hivyo, ukizingatia hoja hii, inaonekana wazi mshangao uliotumika kwenye neno "paa" ambapo mlio uliosikika ghafla ulikuwa wa kushangaza kwa kuona pandikizi la mtu lilikata kichwa kilichoruka na kuashiria suala zima la kifo. Kwa hiyo, katika nukuu mwandishi ametumia motifu "paa" kama nidaa ili kuibua mshangao wa tukio la kifo.

Kwa kuzingatia mjadala kuhusu dhima za motifu "paa" katika makala hii, tunaona mwandishi Kezilahabi ametumia motifu" paa " katika uibuaji wa dhamira ya suala la maisha na kifo. Katika utumiaji huo matokeo yameonesha wazi katika diwani ya *Dhifa* mwandishi ametumia motifu "paa" kama motifu 'pofu' kwa lengo la kuendeleza falsafa ya maisha ilhali katika riwaya ya *Nagona* imetumika kama motifu kuu katika kuibua mchomozo ambao ulizua taharuki kulingana na wingi wa ujitokezaji.

6.0 Hitimisho

Makala hii imechambua dhima za motifu "paa" katika riwaya ya *Nagona* na diwani ya *Dhifa*. Matokeo yameonesha kuwa dhima za motifu "paa" zimegawanyika katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni dhima ambazo zimefanyiwa ukiushi wa kisemantiki na kundi la pili ni dhima ambazo hazijafanyiwa ukiushi wa kisemantiki. Hii inatokana na ubunifu wa mwandishi katika kutumia rasilimali lugha kuibua dhamira mbalimbali. Matokeo yameonesha motifu "paa" imetumika katika miktadha iliyozoeleka na isiyozoeleka na kulifanya neno hili kuwa jipya kulingana na miktadha mipya iliyotumika. Pia, matokeo yameonesha baadhi ya matumizi kurudiwa katika riwaya ya *Nagona* na diwani ya *Dhifa* ili kuibua dhamira ya dhana ya maisha na suala la kifo. Mwandishi ametumia kiwango cha juu cha motifu "paa" katika kusisitiza falsafa ya maisha katika riwaya ya *Nagona* kwa kuwa imetumika kama motifu kuu. Katika diwani ya *Dhifa* motifu "paa" imetumika kama motifu pofu katika kuendeleza falsafa ya maisha. Vilevile, mwandishi ameonesha ubunifu na ukomavu kwa kutumia neno moja katika miktadha tofauti iliyozoeleka na isiyozoeleka.

Makala hii inapendekeza kuwa watafiti wanapaswa kujikita katika tanzu zote za fasihi andishi ili kuweza kuchunguza suala la mchomozo katika msamiati, wahusika, mandhari, matumizi ya alama za uakifishaji, matumizi ya aina mbalimbali za maneno ili kuibua motifu mbalimbali zinazotumiwa na waandishi katika kuonesha ubunifu wao katika utunzi, kuendeleza falsafa au kusisitiza kuhusiana na dhamira katika kazi zao.

Marejeleo

Gaudioso, R. (2014). Kuwako na Wakati Mipaka ya Lugha kama Hatua za Falsafa katika Mashairi ya Euphrase Kezilahabi. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Degli Studdi.

Jilala, H. (2006). *Misingi ya Fasihi Linganishi, Nadharia, Mbinu na Matumizi.* Dar es Salaam: Daudi Publishing Company.

Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (2022). *Dhifa.* Dar es Salaam: Africa Proper Education Network.

Leech, G. N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. Longman. Harlow

Masoud, S. (2015). Matumizi ya Motifu Nambari katika Ngano za Kipemba. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu ha Dodoma.

Massamba, D. P. B. (1983). "Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili." Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi* 55-94, Dar es Salaam: TUKI.

Mbatiah, M. (1998). "Mienendo Mipya katika Uandishi wa Kezilahabi: *Nagona* na *Mzingile*." *Mulika*, Juz. 24, 1–13.

Miall, D. S., & Kuiken, D. (1994). "Foregrounding, Defamiliarization, and Affect: Response to Literary Stories." *Poetics*, 22(5), 389–407. Amsterdam: Elsevier.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi : East African Educational Publishers.

Mulokozi, M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: KAUTTU.

Mungah, C.I. (1999). "Dhana ya Maisha katika Novela Mbili za Euphrase Kezilahabi *Nagona* na *Mzingile*": Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa) Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Njogu, K., & Chimerah, R. M. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi,

Nkwera, F. (1979). *Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing.

Peer, V. W. (1986). *Stylistics and Psychology: Investigations of Foregrounding*. Croom Helm. London.

Ponera, A.S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi.* Dar es Salaam: Karjaner Print Technology.

Rashid, H. (2008). "Ujaala katika Ushairi wa Kiswahili". Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Senkoro, F. (2011). *Fasihi.* Dar es Salaam: KAUTTU.

Simpson, P. (2004). *Stylistics: A Resource Book for Students*. Routledge. London

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi Misingi ya Uchanganuzi Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Press.

Wamitila, K.W. (2013). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Publisher.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya fasihi: Istilahi na nadharia*. Focus Books. Nairobi, Kenya.